


Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 01 Issue: 01 | July-2022

EAJK

# Ukombozi wa Mwanamke Kiuchumi katika Tamthilia za *Kigogo* na *Chema Chajiuza*

**Authors**
**Peter M. Kamau[(1)]; Wandera-Simwa S. Pamela[(2)]**
**Main author email: kamaupkamaum@gmail.com**

**(1.2) Laikipia University, Kenya.**

**Cite this article in APA**
Kamau, M. P., & Wandera-Simwa, S. P. (2022). Ukombozi wa mwanamke kiuchumi katika tamthilia za *kigogo* na *chema chajiuza*. *Eastern Africa journal of Kiswahili*, *1*(1), 26-32. https://doi.org/10.51317/eajk.v4i1.80

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 01.05.2022
Accepted: 02.06.2022
Published: 30.07.2022

**Scan this QR to read the paper online**

**Copyright**: ©2022 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

**Ikisiri**
Utafiti huu umejihusisha na jinsi wanawake wanavyojikomboa kiuchumi katika tamthilia za *Kigogo* na *Chema Chajiuza*. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika iliyoasisiwa na Steady. Akiangazia masuala yanayohusiana na Ufeministi wa Kiafrika. Ufeministi huu hujihusisha na masuala ya wanawake wa Kiafrika kwa kuegemea utamaduni na mapana yake. Ufeministi wa Kiafrika hung'ang'ania kujijenga upya, mawazo huria ya wanawake na kujitegemea wenyewe katika asili zao mbalimbali za kitamaduni. Mihimili ya nadharia hii ni kielelezo katika kumpa mwanamke wa Kiafrika hadhi inayomstahiki kwa kuweka mikakati inayolingana na shida zinazomkabili katika mazingira yake. Kupitia nadharia hii, suala la jinsi wanawake wanavyojikwamua kiuchumi liliangaziwa. Makala husika yalitokana na usomi wa kina. Data iliyopatika kuwa muhimu ilichanganuliwa kupitia njia ya kimaelezo. Data husika ilikusanywa moja kwa moja kutoka maktaba na mtandaoni. Maktaba lengwa ni zile za vyuo vikuu na umma. Matokeo ya utafiti huu ni mwongozo bora kwa jamii nzima hasa wanawake ambao ndio kundi lengwa kujua hatua za kiuchumi wanazochukua wenzao ili kujiweka katika mizani sawa na wanaume.

**Maneno muhimu:** Usawa, ukombozi, mwanamke, mwanamume, kiuchumi.

## UTANGULIZI

Katika utafiti huu tumeangazia mapitio ya maandishi muhimu kuhusu jinsi wanawake wanavyojikomboa kiuchumi. Kisha tukaangazia suala la nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ambayo imekuwa mwongozo wa uchunguzi wa utafiti huu. Baadaye utafiti wetu ulifuatiwa na uchanganuzi wa deta iliyokusanywa kutoka tamthilia ya *Kigogo* na *Chema Chajiuza*. Matokeo ya utafiti yalikamilishwa kwa hitimisho iliyozungumzia kwa muhtasari suala nzima la utafiti.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Kwa miaka na mikaka, wanawake wamepigania usawa katika masuala ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kitamaduni. Utetezi huu umekuwa mwanga wa kuzindua wanawake kutoka ukandamizaji hadi ukombozi unaowaweka katika kilele sawa na wanaume. Usawa huu ulichochea kufanyika kwa utafiti ili kuonyesha namna wanawake walivyojikomboa kiuchumi na kuwa mihimili mikuu katika familia. Uwezo huu wao unaonyesha tofauti na mitazamo ya kikale ambayo ililenga kuonyesha jinsi mwanake alivyonyimwa haki ya kumiliki mali waliochuma au urithi.

Wanawake wa kisasa wameleta mageuzi kwa kuonyesha ushindani sawa na wanaume katika kuchuma na hivyo kuleta mabadiliko yanayowapa nguvu sawa kiuchumi na wanaume. Beauvuor de (1949) anaeleza kuhusu mwanamke anayesema kuwa hajawahi kumtegemea mwanamume katika maisha yake. Amefanikiwa kiuchumi peke yake kwa kuchuma mali kwa nguvuze. Anajivunia kwa kujitosheleza yeye binafsi maishani. Wanawake ni wachumi sawa na wanaume wanapopata fursa. Mwanamke huyu alijitoma katika uwanja wa kusaka mali na kufaulu. Baada ya kujitosheleza aliziba mwanya wa utegemezi kwa kuwa mfadhili wa mahitaji yake. Hii ndiyo nafasi wanawake wanayowania.

Mbinu ya kuwainua wanawake kiuchumi ni kigezo mahususi cha kuwakomboa kutokana na matatizo mengi yanayowakumba. Serikali pia huwa na jukumu la kuona kwamba kila mwananchi ana uwezo kiuchumi wa kujitegemea. Mburu (2016), katika utafiti wake anaonyesha vile wanawake wanavyojitegemea wanapofanya biashara zao ndogondogo. Anasema kuwa wanawake wameweza sio tu kujiinua kiuchumi bali pia kuimarisha misingi ya kijamii. Wanawake wanaojiingiza katika biashara ni wengi ikilinganishwa na idadi ya wanaume ambao wamekuwa wakifanya biashara kwa miaka mingi. Wanawake wameweza kwa kiasi kukabiliana na matatizo yanayotokana na ugumu wa kuanzisha biashara na kuyashinda na hivyo kuweza kujimundu katika kazi zao. Kuwaelimisha katika masuala ya biashara kunawasaidia sana kujiinua na kujiendesha.

Serikali ya Kenya inamdhamini mwanamke. Sheria zimeundwa ambazo zinawapa wanawake haki ya kumiliki mali kama vile mashamba ambayo ni kitega uchumi hapa nchini. Pia imeweka utaratibu wa kuwawezesha kupata haki ya urithi wa mali. Ardhi hii ni muhimu kwa wanawake waekezaji, World Bank (2007). Pia serikali imejisatiti kwa kuunga makundi ya wanawake yaliyo na lengo la kuwainua kifedha. Makundi haya hutoa fedha kwa riba nafuu kwa nia ya kuwavutia wanawake wengi kuanzisha biashara zao bila masharti magumu. Serikali nayo huwatilia ponjo kwa kuyatambua makundi haya kwa kuweka sheria za kuyalinda kwa lengo la kuyaimarisha ili kuhudumia wanawake wote nchini. Mfuko huu wa fedha umetengewa wanawake ili kuwakwamua kiuchumu. KWFP ni shirika ambalo linawasaidia wanawake wa Kenya kukopa fedha. Wanawake hujiunga katika makundi mbalimbali ili kuweza kukopa fedha hizi wakidhamirilia kujiinua kiuchumi, Stephenson na St-onge (2005).

Wanawake wanawajibu kwa kutekeleza majukumu ili kujikwamua na kufikia malenga ya kiuchumi. Wamejitokeza kufanya kazi za kila sampuli. Kujipenyeza katika kufanya kazi kunawaondolea lawama kuwa ni walaza damu wanaotegemea wanaume. Sharif (2017) anaeleza jinsi uwajibikaji kazini wa wanawake umekuwa kigezo cha kujikimu maishani. Anamrejelea mhusika Bi. Farashuu anayefanya biashara ndogondogo kama vile kutunga vikuba na asumini, kusukuma mikate, vitumbua na kadhalika katika juhudi zake za kujitegemea kiuchumi. Kazi za sampuli hii huwakidhia wanawake mahitaji yao kifedha. Katika kufanya kazi, pengo baina yao na wanaume huendelea kupungua. Hatima ya mambo ni kukuza kazi zao hadi kufikia kiwango cha kupata mtaji mkubwa unaowawezesha kujitegemea.

Syekei (2017) anaangazia suala la wanawake na uchumi kwa kueleza jinsi wasichana wanavyochangia kukimu

wazazi wao kabla ya kuolewa. Sawa na wavulana, wasichana wamekuwa wakitegemewa kupunguza makali ya shida nyumbani. Aidha, husaidia katika majukumu kama vile kusaka chakula, kuwasaidia kifedha, kuwatunza ukongweni na mengine. Pia wanapoolewa wanakuwa tegemeo kwa mume katika kuchuma. Hutembea mbega kwa mbega na waume wao kwa kutekeleza majukumu yao pamoja.

Katika utafiti huu, tumetumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Nadharia hii iliasisiwa na Steady (1981). Kwa kushirikiana na wengine waliweza kuanzisha nadharia hii ili kushughulikia wanawake wa Kiafrika hasa katika bara la Afrika. Nadharia hii huangazia masuala yanayonuia kumkomboa wanamke kutokana na dhuluma za kila aina yanayotokana na jinsia ya kiume. Kabla ya kuasisiwa nadharia hii, wanawake wa Kiafrika walikuwa wakibaguliwa katika ulingo wa kimataifa. Ndiposa ukazuka mlengo huu ukiwa na lengo la kuwapa usemi kwa kushughulikia matatizo yao wenyewe. Nadharia hii huongozwa na mihimili ifuatayo;

1. Hutetea usawa wa mwanamke kama mwanamume katika jamii.
2. Kuhamasisha utambulisho wa wanawake ambao hawategemei wanaume wajitokeze.
3. Hukuza na kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama wadhulumiwa na kusaka utambulisho.
4. Kuzindua ari kwa wanawake kifasihi na uhusiano wao na wanaume katika jamii.

Katika utafiti huu tumetumia mhimili wa kwanza ambao unalenga kusawazisha usawa kati ya wanawake na wanaume katika jamii. Watafiti wameonyesha jinsi wanawake wanavyochukua hatua za kiuchumi ili kufikia kilele cha usawa na wanaume.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Ukombozi wa Mwanamke Kiuchumi

Uchumi ni mfumo wa mtu anavyoweza kufanya ili kupata mapato yanayomwezesha kujitegemea. Ni hali ya kujiweza katika kutimiza mahitaji ya mtu kifedha. Watu ambao wana uwezo wa kifedha huwa mabwenyenye wanaopewa heshima kutokana na nguvu zao za kuchuma. Vivyo hivyo katika familia, aliye na uwezo wa darahima huabudiwa ili mtegemea nudu aendelee kunufaika. Hufanya hivi ili asiukate mrija uletao shibe. Mtaji katika familia umekuwa ukiendeshwa na wanaume ambao wanajulikana kama wamiliki wa mali. Wao ndio husaka na kukidhi mahitaji ya familia. Wanawake wengi huachwa nyumbani wakishughulikia masuala ya utunzi wa mali iliyochumwa na waume wao. Hali hii huwafanya wanawake wategemezi. Kutokana na hali hii, wanawake wamepiga hatua kwa kujitoma katika bahari ya uchumi ambapo hatua wanazopiga wanaume, ndizo wanawake wanazopiga. Katika kuchuma, wanawake wamejtokeza katika hali mbalimbali.

### Biashara

Wanawake wa kisasa wanajihushisha katika kufanya biashara mbalimbali kama wanaume. Biashara nyingi hufanyika nje ya makazi na hivyo kumilikiwa kwa mapana na wanaume huku wanawake wakisalia nyumbani kulea watoto na kufanya kazi pale. Mwanamke wa sasa ametoka nje na kuanzisha biashara ambazo zinampa pato sawa na mwanamume. Katika tamthilia ya *Kigogo*, Sudi akizungumza na Boza katika karakana ya kuchongea vinyago anasema,

*Sudi: (Akimnyoshea kidole.) Chunga ulimi wako! Tangu lini maembe ya Ashua yakanuka,*
*eh? Si wewe hapa uliyeniambia hakuna anayeuza maembe matamu kama Ashua katika*
*soko hili?(uk 1)*

Usemi huu unamrejelea Ashua mkewe Sudi ambaye anajihusisha na biashara ya kuuza maembe sokoni. Anamsaidia mumewe katika kukidhi mahitaji ya kimsingi ya familia. Anapunguza mzigo alionao mumewe wa kusaka kwa niaba ya aila, mzigo ambao kwa kawaida huachiwa wanaume kushughulikia.

Wanawake wanaonyesha kuzinduka kutoka lepe la usingizi kwa kuwazia mustakabali wa kesho kwa kufahamu kuwa uwezo wa wanaume katika kuchuma hauna miujiza yoyote. Huwa ni kukazana na kupigania nafasi zilizoko. Msingi wa familia imara hujengwa katika msingi wa mapatano katika kikidhiana mahitaji. Hali ya kuwa mtu mmoja ndiye mwenye uwezo wa kumiliki mali ni hali ya kutia familia taabani. Hili linatokana na kwamba mhimili wa mkidhili haja pale nyumbani unaposambaratika ni kumaanisha kuwa nao msingi wa familia utayumba. Kuyumba huku huleta maafa na majuto. Majuto haya huja na matatizo mengine kama talaka ambapo wanamke huwa katika hali ya mfadhaiko wasijue la kufanya. Nao watoto katika hali ya kukosa malezi ya wazazi, msingi wao wa maisha ya kesho huwa umegonga ukuta.

Pia wanawake wamejitoma katika biashara za ulevi ambazo humilikiwa na kufanywa sana na wanaume. Asiya anawauzia wanaume na wanawake pombe katika klabu anachomiliki katika eneo la Mangweni. Tazama mazungumzo katika tamthilia ya *Kigogo*.

*Tunu: Koma! Unajua ni hatia kuuza pombe haramu?*

*Ngurumo: (Anaendelea kucheka.) Wewe Tunu, unavuka mpaka sasa. Unatarajia sisi tujiburudishe na nini au tuende tukaibe?*

*Sudi: (Kwa hasira.) Hujalijibu swali la Tunu.*

*Mamapima: (Kwa hasira.) Nina kibali*

*Ngurumo: Kutoka kwa serikali ya Majoka bila shaka! (uk 61)*

Wanawake hawachagui kazi. Kazi ya kumiliki na kuuza klabu ni kazi ngumu hususani kwa mwanamke ambaye kwa nguvu za kimwili anachukuliwa kuwa dhaifu. Kwanza, wanawake hawaruhusiwi kufanya kazi hii ya kumiliki vilabu na kushiriki ulevi kiholela katika utamaduni wa mwafrika. Maisha haya ni ya wanaume hususan baada ya kazi wakati wanawake wanapika na kushughulikia watoto jioni. Jambo la shani ni kwamba klabu hiki kinamilikiwa na Asiya ambaye anapata kipato chake kutokana na uuzaji wa pombe. Anawekea kazi yake ulinzi wa kutosha kwa kuwafurusha wanaojaribu kumharibia biashara yake. Tazama katika tamthilia ya *Kigogo* anaposema,

*Mamapima: Ona sasa! Mnaniharibia biashara. Nimewapa dakika moja tu mwione Nyumba hii paa. Nikiwapata hapa, mtajua kwa nini wananiita Mamapima.* (uk 62)

Asiya hategemei yeyote kuwa mlinzi wake. Ukakamavu wake unamfanya kuogopwa na hivyo kazi yake kupewa heshima na kila mtu anayefika katika klabu chake kwa nia ya kujiburudisha. Anawatishia wanaume na wanawake ambao anasema nia yao ni kumharibia biashara yake. Katika sakata hii, Tunu, Sudi na Siti inawabidi kunywea na kuondoka kutokana na vitisho vya mwanamke huyu asiyetetereka katika msimamo wake.

**Kufanya Kazi**

Kazi za kibarua cha kila siku ni njia moja ambayo wanawake huitumia kijiiunua kiuchumi. Ushahidi unajitokeza wakati Nabaganzi anapoamua kuikata minyororo ya utamaduni kwa kumweleza mumewe kuwa yuko tayari kufanya kazi ili kuokoa familia yake ambayo inatishio la njaa kwa vile mumewe ameshindwa kuwakimu. Tazama katika tamthilia ya *Chema Chajiuza.*

*Nabaganzi: Mimi nitamwendea Kwatampola. Nataka nipate kazi ya kubebe mchanga. Nataka angalao nipate chajio kwa wanangu. Sipo tayari kuwazika nigali mchanga… (uk 83)*

Ubaguzi wa kazi kulingana na jinsia hauna mashiko kwa mtazamo wa Nabaganzi. Hii ni kazi ya ujenzi wa nyumba. Kazi hii inajulikana kuwa ni ya wanaume. Mwanamke huyu anaamua kujiunga na wanaume katika kazi hiyo ili aweze kuwalisha watoto wake. Katika kufikia kiwango hiki mwanamke huyu ameona kuwa mumewe Bakehena hana uwezo wa kuwalisha ama kuwatimizia mahitaji yao. Anakashifu kitendo cha mumewe cha kumwibia tajiri wake na kumjengea nyumba ya kifahari. Baada ya kitendo hicho mabwanyenye walikataa kumpa kazi na hivyo akabaki akitaabika asiweze kulisha familia. Wanawake wanastahili kujitokeza kwa kujifanyia kazi kwa nguvu zao bila kubagua. Mama huyu amejikwamua kutoka kwa utumwa wa utegemezi wa mume kuwapa mahitaji yao. Amejiweka katika miguu ya mume kuongoza familia hii ambayo Bakehena ameshidwa. Anaenda kuomba kazi kwa Kwatampola ambaye ni hasimu wa mumewe. Nabaganzi anasema kuwa Kwatampola amempa tayari shilingi elfu tano ambazo walitumia siku iliyotangulia huku Kuni akimwongezea maharagwe.

Uwezo huu wa kufanya kazi kwa wanawake huwa na usuli wake kutoka utotoni. Kazi ambazo wasichana hufunzwa pale nyumbani huwaelekeza katika kujitegemea katika maisha ya baadaye. Wanapoolewa, nguvu hizo hudhoofishwa na waume zao wasioweza kukimu kila kitu ili kuonyesha udhibiti wa mambo pale nyumbani. Kwa wanaume weledi, nguvu hizi huendelezwa ili kuwasaidia katika mzigo mkubwa wa familia. Ndiposa inadhihirika kwamba wanawake huwa wanajitegemea hususan kabla ya kuolewa. Na isiwe ni itikadi, wake kulaza damu waolewapo kwa kuacha kazi zao na kumtegemea mume. Kutokana na wazo hili inafahamika kwamba Nabaganzi alikuwa na kazi yake ambayo aliiacha baada ya kupata mume. Anasema haya katika tamthilia ya *Chema Chajiuza.*

*Nabaganzi: Nisahau nini hapa. Una nini ambacho ulininunulia nikisahau? Kila nilicho nacho nilijinunulia nilipokuwa nyumbani kwetu. Shauri yako. Mkahawa wangu ulinifaa. Laiti ningejua singetaabika… (uk 85)*

Wanawake katika mazingira ya nyumbani huwa mkongojo kuwasaidia wanaume kwa kuwapa hadhi. Mchango wao hufunikwa katika kivuli cha waume wao kuwa ndio wenye kumiliki mali. Nabaganzi anadhihirisha kuwa amefanya mengi katika nyumba ile kwa kununua vitu vingi. Anamshtumu mumewe kuwa hana chochote alichonunua ndani ya nyumba ile. Ikiwa ni kuondoka na kuchukua kilicho chake, angebeba takribani vitu vyote. Vitu wanavyomiliki ni vile mwanamke huyu alikuwa amenununa alipokuwa kwao. Hivi anamaanisha hana chochote alichoweza kununua baada ya kuolewa na Bakehena zaidi ya watoto wawili alio nao. Kiuchumi alikuwa na uwezo mkubwa ambao kwa sasa ni kama umedhibitiwa kwa kufugwa nyumbani asiweze kufanya kazi ya kumpa pato lolote. Kabla ya kukutana na mumewe alikuwa mmiliki wa mkahawa. Hii ni kazi ya nje ambayo inafanywa na wanaume.

Jamii ya wanawake haichagui kazi. Ushindani huu ndio unaomfanya mwanamke kuwa mke halisi anayejitegemea. Anajuta kuacha kazi hii yake na kunyenyekea kwa mume asiyemweza kwa mahitaji anapoolewa. Ndoa inawaletea wanawake matatizo kwani inawazima ari ya kujiendeleza. Nabaganzi anaona ajitegemee tena kwa kujifanyia kazi mwenyewe na kuendeleza maisha yao. Hivi anakiuka masharti ya mumewe kubakia nyumbani kama inavyodhirika katika tamathilia ya *Chema Chajiuza.*

*Nabaganzi: …Nilipofikiria nikaona njia pekee ya kujikomboa kama mwanamke ni kutafuta kazi nijitegemee ilivyokuwa awali. (uk 89)*

Wanawake hujifunza kazi mbalimbali kabla ya kuolewa na kutoka kwa wazazi wao. Wazazi wanapowalea watoto wao, huwafunza kazi za kila nui. Hali ya kujitegemea huanzia pale nyumbani hata wasichana. Wanapoolewa, wao huacha kazi zao ilikuchukua majukumu waliyotengewa na mume nyumbani huku mume akitoka nje kusaka tonge. Kazi ambayo mwanamke alikuwa akifanya inastahili kuendelezwa kwa manufaa ya kumwauni mume, mambo yanapoenda kombo. Nabaganzi anajikomboa kimawazo anapowaza kujitoa kimasomaso kufanya kazi ili kuokoa maisha yake. Mwanamke anaweza kujikomboa kwa kufanya kazi. Kazi hii ni ile inayofanywa hata na wanaume.

**Kilimo**

Kilimo ni kigezo cha kutegemewa katika kukimu mahitaji mengi ya familia. Ni njia muhimu katika kupata lishe na mapato kutokana na mauzo ya bidhaa kutoka mashambani. Uwezo wa wanawake wa kufanya kazi ulikuwa umezikwa katika utamaduni wa kuamini kuwa wanaume wana jukumu la kukimu. Hivyo kazi kwa wake sio suala muhimu na hivyo kuwafanya wazembe. Wanawake wanalaumiwa kwa kuwa dhaifu kwa ardhi ilimilikiwa na wanaume. Kujihusisha katika kilimo ni ari ya ukombozi kwa kujifanyia kazi wakiwa bado kwa wazazi wao. Wanalima mashamba ambayo mazao yake yanawasaidia wazazi na wao wenyewe. Kuni anajihusisha katika kilimo kama inavyodhihirika katika tamthilia ya *Chema Chajiuza*.

*Kuni: Mama ana kishamba. Ukikubali tunaweza kuanzia pale. Nilipomwambia hali yetu alituhurumia aka… (uk 5)*

Kuni anamrejelea mama yake kama mmiliki wa shamba. Shamba hili linalimwa na kuauni hali ya familia. Sasa anaona kuwa shamba hili wakiweza liwekeza litawasaidia kuondokana na hali ngumu wanayoipitia. Ardhi ni muhimu ili kuwainua wanawake na kuwafanya wamiliki mali. Kuni anasema kuwa kishamba hicho alikuwa anakitumia kabla ya kuonana na Kwatampola. Ardhi ni kitu adimu kumilikiwa na wanawake. Wanaume wenye uwezo mwingi humiliki mashamba makubwa. Wao huonekana kama matajiri. Vivyo hivyo, wanawake wanaomiliki mashamba huonekana sawa na wanaume. Mamake Kuni kumiliki shamba na kuwauni kwalo ni ishara ya upevu ambao Kwatampola hajaufikia kwani hamiliki hata kiota cha ndege.

Uwezo wanawake kufanya kazi kama wanaume unadhihirika katika usemi wa Kuni kuwa ana uwezo wa kujijengea nyumba kwao. Katika tamthilia ya *Chema Chajiuza,* Kuni anasema,

*Kuni: Nami ninaweza kujijengea kwetu Bukinda Kabale nikaisha huko. Nitaanza maisha mapya ya mwanamke kujitegemea. Pesa zangu… (uk 78)*

Ardhi inajitokeza kuwa na umuhimu maradufu kwa wanawake. Wanawake kuwategemea wanaume kuwakimu ni kuzembea wakiwa na nia ya kulaza damu wakistareheka. Kuni anaona pesa atakazopata kutokana na kipande cha shamba kitamwezesha hata kujenga nyumba kwao. Mwanamke wa kisasa anafanya kazi kama mwanamume. Kuni anadhamiria kujijengea nyumba kwao ambayo kwa miaka kumi sasa Kwatampola hajamjengea. Uwezo wa Kuni unaonekana kuwa bora kuliko wa mumewe. Uwezo huu ni ukwezo unaodhihirisha kuwa wanawake wanaweza kuishi peke yao bila kuwategemea waume wao. Wanaweza kuchukua majukumu ya wanaume na kuyatekeleza kikamilifu. Hali hii ndiyo inayowafanya wanawake kuchukua nafasi ya wanaume ambao wameshindwa kukabiliana na majukumu yao ya kila siku huku wanawake wakijibwaga katika uwanja wao na kuwashinda. Mabadiliko ya kiuchumi hujitokeza wazi pale wanawake wanapojitokeza kwa nia ya kujitegemea.

Suala la wanawake kurithishwa mali mume anapofariki ni wazo la kuwawezesha kujitegemea aushini. Mumewe Hashima anaweza kujikimu kiuchumi na kishamba cha mumewe. Tazama katika tamthilia ya *Kigogo.*

> *Hashima: Wapi? Kichele hiki tu, hata hakipikiki mkate wa sinia. Sijui tutakula nini*
> *tukingoja soko lifunguliwe. (uk 52)*

Chakula cha kulisha familia kinapatikana kutokana na juhudi za kazi anayoifanya. Anaona chakula ni haba kutokana na kiangazi katika eneo ambacho kulififisha mazao. Anaonyesha manufaa ya ardhi katika kukimu maisha yake na mtoto wake Tunu kabla ya kufunguliwa soko ambapo mtaji wa mapato utaongezeka.

**Urithi wa Mali**

Mwanamke wa Kisasa kurithishwa mali ni ukwezo wa kumpa nguvu za kiuchumi. Mzazi wa kisasa hana budi kumnyoshea mwana msichana mkono wa mali anayomiliki akiwagawia wavulana. Kuni anadhibitisha kuwa yeye ni mmiliki wa ardhi kwao katika tamthilia ya *Chema Chajiuza* anaposema,

> *Kuni: Nami pesa zangu nazitaka lakini si kwa matumizi yake. Kwetu nina pa kujenga.*
> *Kazi siwezi kuiacha ingawa sitarudi kwake. Niweze kujitegemea. (uk 78)*

Wanawake wanajiweza. Usawa wa ugavi wa mali unawaweka wanawake mbele sana ya mwanamume katika kupigania usawa wa jinsia. Sera ya kuwagawia wasichana mali imewafaidi sana kuona kwamba msichana anakuwa mmiliki wa mali kwao na kwa mume. Anapoolewa kile anachomiliki mume kinakuwa chao wote wawili. Hii ndio sababu Kuni anasema kuwa pesa ni zake ila sio zake na mumewe. Sababu hii ndiyo inayomfanya Kuni aseme kuwa angejenga kwao ili aweze kuishi huko peke yake ingawa alikuwa akimlazimisha Kwatampola ashiriki wizi ili amjengee nyumba waishi peponi. Katika kutafuta kazi, Kuni anasema hawezi kuacha kufanya kazi kwani ndipo anapopata kipato chake. Ataweza kujikimu katika maisha yake. Wanawake wanachukua njia mbadala katika ndoa kwani kile achumacho ni chake na kile mume anachochuma ni chao. Wanaume wanakuwa kwa kiwango fulani watumishi wa wanawake. Inawahitaji wanaume kutia juhudu za mchwa kujitegemea na kujiweka katika ulingo halisi wa mwanaume ili kuishi na wake zao kwa usawa. Hali hii ya wanawake kumiliki mali inadhibitishwa katika tamthilia ya *Chema Chajiuza,* Kwatampola anaposema yafuatayo.

> *Kwata: … Ninakumbuka, nilipompata, alikuwa na shamba lake Bukinda, Kibale. Aliuza*
> *muhogo na viazi sokoni Mwanjari kila Alhamisi. Kipawa kakisahau. Mara tu*
> *nilipomwingiza nyumbani sijui lililomfika? (uk 98)*

Ni wazi kwamba uwezo wa kiuchumi kwa wanawake huwepo kabla ya hata kuolewa. Wazazi kwa pamoja na kampeni ya serikali imewezesha wanawake kukwamuka kutokana na kuwekwa kando katika sera ya umilikaji ardhi. Wanaume ambao wanawaheshimu wasichana wao huwagawia mali ikiwemo vipande vya ardhi wanapowagawia wavulana sehemu zao kama urithi. Sio ardhi pekee, wanawake wanarithishwa mali sampuli kama vile nyumba, magari, biashara wanayoachiwa na wazazi wao kujiendeleza. Wanaume wa aina hii huwawezesha kuwafunza wanaume wenzao katika jamii kuwa wasichana na wavulana wote ni sawa. Mchango wa wanaume hawa ni kichocheo kuwa wanawake wanaweza miliki mali na hamna laana katika kitendo hicho. Hili ni funzo ambalo wanawake wanastahili kufunzana huku wakishauriana na wanaume kugawia kila mtu mali yao kwa usawa awe mvulana au msichana. Hii ndio sababu

Kwatampola anasema kuwa Kuni alikuwa mmiliki wa shamba ambalo alikuwa analima huku akiuza mazao yake cheteni. Kwatampola anaona wakati huo ulikuwa afadhali kwa Kuni kuliko sasa. Ndoa ilimnyima fursa ya kuendelea kufanya kazi yake kwa nia ya kumtegemea mumewe. Ardhi hii kwa wanawake ina manufaa ili kujijenga kiuchumi.

**Kandarasi**

Hii ni kazi ya mkataba wa malipo katika kipindi fulani cha wakati. Mwanamke wa sasa anafanya kandarasi kama njia ya kujiongezea pato. Kuzinduka kwa wanawake kunakuwa faraja katika familia wanapojihusha na miradi ya kitaifa. Kitendo hiki kinatia moyo wanaume kwa kukionea fahari na kukipokea kwa mikono mikunjufu. Boza anafurahia kazi ya mkewe katika tamthilia ya Kigogo. Ananukuliwa akisema,

> *Boza: (Anaipokea keki huku akichekacheka.) Keki, keki ya taifa. Imeokwa na mke*
> *wangu mwenyewe! Karibuni. (uk 13)*

Boza anatambua juhudi za wanawake na mchango wao katika taifa. Anafuraha kuwa mkewe amefanikiwa katika kuoka keki ambazo zitaliwa kusherehekea siku ya kupata uhuru wa Sagamoyo. Hii ni ishara ya kuunga mkewe mkono katika kazi yake badala ya kulaza damu akingojea kile ambacho mume atachuma. Mwanamume huyu anamwona mkewe kama mshirika katika mahitaji ya nyumbani na wala sio msaliti wa majukumu kwa kumwachia mumewe.

Kuyumba kwa misingi ya ndoa kumewazindua wanawake wengi ambao walikuwa waadhiriwa kutokana na kugubikwa na utamaduni uliowafanya wategemezi. Mwamko wao kutaka kuwa wahusika katika maisha yao ya usoni, kunazua mwamko mpya ambao unawakomboa kutoka mitazamo finyu ya maisha yao. Ndiposa wanawake wametia miguu yao katika kusaka mali kwa kujiingiza katika majukumu ambayo awali yalifikiriwa kuwa ni kazi za wanaume. Fedha wanazochuma ndizo zinawasaidia kusimama wima wakati wanaume wanapowatenga au kuwatelekeza.

Asiya, mkewe Boza anapewa kandarasi ya kuoka keki za kitaifa. Hii ni ishara ya uwezo wa wanawake katika kujihusha na masuala ya kitaifa. Ni ishara kuwa wanawake hawajadhibitiwa katika kuchangia majukumu ya nje zaidi na yale waliyotengewa ya nyumbani. Uwezo wao unatambulika kutokana na juhudi wanazotia katika kazi zao.

**MAHITIMISHO**

Wanawake wana uwezo wa kiuchumi sawa na wanaume. Malengo yao ya kutaka kujitegemea yanaweza fikiwa kwa kujitokeza kufanya kazi mbalimbali ambazo zitachangia kupata mapato ili kutatua shida zao. Matokeo ya utafiti yanaonyesha wanawake wanaopata nafasi ya kuchuma huwa mstari wa mbele kutimiza majukumu ya kifamilia vyema kama wanaume. Wao huweza kushughulikia mahitaji ya watoto vyema zaidi. Ni wazi kwamba huwapunguzia wanaume mzigo wa mahitaji. Wanawake wa kisasa wana jukumu la kuchangia katika maendeleo yao, familia na nchi kwa kujitokeza kupigania nafasi zao kikamilifu. Wachume bila kubagua kazi. Pamoja na hayo, wameonyesha kushiriki vyema hata katika kazi zinazoaminika ni za wanaume. Waandishi wa tamthilia zote mbili wameonyesha kwa hakika kuwa wanawake wana uwezo sawa na wanaume katika nyanja zote za kiuchumi.

**MAREJELEO**


Beauvoir, S. de. (1949). *The second sex*. Pan Books.

Mburu, P. W. (2016). *Selected factors that influence performance of women-run publishers*.

Sharif, J. F. (2017). *Kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya ya Small enterprise in Langat Sub County, Kenya* [Thesis, Laikipia University].

Steady, F. C. (1981). *The black woman cross-culturally*. M. A. Schenkman.

Stephenson, L., & St-Onge, A. (2005). *Support for growth-oriented women entrepreneurs in Kenya*. http://www.kwtf.org

Syekei, M. N. (2017). *Nafasi na athari ya kiongozi wa kike katika tamthilia teule za Utengano na Kamwe si Mbali Tena* [Thesis, Chuo Kikuu Cha Huria Tanzania].

World Bank. (2007). *Gender and economic growth in Kenya*. http://www.greenpressinitiative.org